**MKOA WA KUSINI** **TAREHE:16/3/2026**

**WILAYA YA MUHANGA** **ALAMA: ………./100**

**MUHULA WA PILI** **MUDA: MASAAHA MATATU(3)**

**KIDATO CHA PILI**

**<u>MTIHANI WA KISWAHILI</u>**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yaliyoulizwa .**

Majira ni kipindi maalumu cha hali ya hewa.Majira haya ndio huelekeza upanzi wa mimea na uvunaji wa mazao hapa kwetu. Tupo na majira mbalimali.Yapo majira ya mvua nyingi.Majira ya mvua nyingi ya mfululizo huitwa masika.

Majira haya hutokea kuanzia mwezi wa Machi hadi Mei kila mwaka.Shughuli za kupanda mimea kama vile maharagwe ,mtama,mbatata,mahindi na kadhalika hutokea mwanzoni mwa majira ya masika.Mimea hiyo huota na kupaliliwa katika majira haya ya masika. Vilevile, mimea mimea mbalimbali kama vile mikahawa,mipareto,migomba,minanasi na kadhalika hustawishwa mnamo majira haya.

Msimu huu wa masika hufuatwa na majira ya kiangazi au ukame.Huu ni wakati ambapo jua kali huwaka,mvua hukosa kunyesha na ardhi hukauka.Yapo majira mafupi ya kiangazi ambayo hutokea kuanzia Juni hadi Septemba.Mifugo na mimea hukosa chakula na maji ya kutosha na huanza kuwa na afya mbaya mnamo majira haya. Baadhi ya wakulima huanza kuvuna mazao yao katika majira ya kiangazi.Wengine hulima na kuandaa makonde yao mnano majira haya kabla ya mvua kunyesha.

Mbali na majira haya,yapo majira ya vuli.Huu ni wakati ambapo huwepo mvua ndogondogo tu.Majira haya hutokea katika miezi ya Novemba na Februari.Wakati wa vuli,wakulima hupanda vyakula vinavyochukua muda mfupi kukua na kukomaa.Hata hivyo, shughuli nyingi za upanzi hazifanyiki kwa kuwa mvua inyeshayo huwa haitoshi kukuza baadhi ya mimea.

Hali kadhalika,yapo majira ya kipupwe.Kipupwe ni majira ya baridi ambayo hutokea katika miezi ya Septemba na Novemba nchini Rwanda.Wakati huu wa mwaka huwepo baridi kali na hubidi watu kuvaa sweta,makoti na hata makabuti.

Kwa ufupi,wakulima wengi nchini Rwanda huzingatia majira mbalimbali wanapofanya shughuli zao za kilimo.Wao hutegemea mvua na jua katika kukuza mimea.

**SEHEMU YA I:UFAHAMU/alama 20**

1**.Eleza maneno yafuatayo kutoka kwenye kifungu.(alama4)**

a)Masika……………………………………………………

b)Kivuli……………………………………………………

c)Kiangazi………………………………………………………….

d)Kipupwe…………………………………………………………

2.Taja majira ambapo huwepo mvua ndogondogo**.(alama3)**

**………………………………………………………………**

3.Ni katika majira yapi ambapo jua kali huaka nchini Rwanda?**(alama3)**

**……………………………………………………………………….**

4.Toa mifano minne ya mazao yapatikanayo  nchini Rwanda**.(alama4)**

**………………………………………………………………………….**

5.Taja jina la majira ya baridi  nchini Rwanda**.(alama3)**

**…………………………………………………………………………**

6.Tunga sentensi moja sahihi kwa kila neno:**(alama3)-**

a.Novemba…………………………………………………………..

b.Mvua…………………………………………………………………….

c.Nanasi…………………………………………………………………….

**SEHEMU YA PILI:SARUFI /ALAMA 65**

**7.Tunga sentensi sahihi moja kwa kila Kivumishi:(Alama 5)**

a.huyu…………………………………………………

b.Mzuri…………………………………………………….

c.Wangu……………………………………………………….

d.Yupi………………………………………………………….

e.Watano**………………………………………………………….**

8. **Tumia o-ote kujaza sentensi hizi**: **(alama 2)**

i. Nitatumia jembe……………………..

ii. Niletee machunga …………………….

**9. Chagua jibu sahihi kati ya yale yaliyomo mabanoni. (alama 5)**

a) Mwaka huu tumepanda mbegu…………….. (**nyingi, wengi, mingi)**
b) Masokwe ………………………………wanacheza porini. **(masita, saba)**
c) Ngamia ………………………………**(mbili,wawili)**
d) Wanafunzi ………………………wamefika( **wote, bote)**
e) Mtoto ………………….ameenda wapi? ( **wengine, mwingine,mwingineo)**

**10.** Tumia majina haya ya vifaa vya shule kwa kujaza sentensi hizi:**kalamu,kifutio,chaki, dawati na rula.(alama5)**

a.…………………. hutumiwa kwa kufuta ubao.

b.Hutumiwa kuandika daftarini.Ni...................

c..........................hutumiwa kwa kuandika kwenye ubao.

d.................................ni kifaa kinachotumiwa kwa kukaliwa na wanafunzi.

e...................hutumiwa kwa kupiga kistari.

**11. Andika sentensi zifuatazo katika hali yakinishi au hali kanushi.(alama5)**

a.Mama anapika chakula. ……………………………………………………..

b.Yeye hachezi kabumbu……………………………………………………….

c.Wao hawasomi vitabu……………………………………………………….

d.Baba anakula maharagwe……………………………………………………

e.wewe hukunywa chai jana……………………………………………………

12. Andika aina tatu za nomino unazozijua **(alama3)**

i) ………………………

ii)……………………….

iii)…………………….

**13. Sema aina za vivumishi kwa maneno yaliopigiwa mistari kwa sentensi zifuatazo .(alama10)**

a.Mtoto **huyu** anacheka………………………………………….

b.Mpira **wangu** umepasuka………………………………………

c.Muhoga **upi** ni wangu ?……………………………………

d.Kuku hawa wametaga mayai **machache**…………………………………….

e.Kitamba **cheupe** kimeraruka…………………………………..

**14. Jaza jedwali hii: (alama10)**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| a.Kielezi | ………………………… |
| b.Ng'ombe | …………………………. |
| c.Kondoo | ………………………. |
| d.Zizi | ………………………… |
| e. ………………….. | Wauzaji |

**15. Tambua aina za nomino kwa maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo :(Alama 5)**

a. Tutaenda kuzuru nchi ya **Rwanda** lini?

b.**Kigali** ni mji una majengo mengi sana

c.**Ng'ombe** inatupa maziwa.

d.Kila **mwanafunzi** anapaswa kuleta karatasi ya kufanyia mtihani.

e. **Gasimba** ni mwanafunzi mwerevu.

16. Chagua jina linalofaa kwa kujaza sentensi hizi:**pundamilia,sokwe-mtu,tembo,twiga,ng'ombe.**
**(alama 5)**

a.Huwa na akili inayokalibiana na ya mtu.Yeye ni……………………………

b.……………………….huwa na milia myeupe na myeusi katika mwili mzima.

c.Ndovu huitwa pia…………….. ……………..

d.…………………………hukamwa na kutoa maziwa.

e.Huwa na shingo ndefu sana na ndiye mrefu kuliko wanyama wengine porini.Yeye ni…………………..

**17. Taja kinyume cha vielezi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo: (alama 4)**
a) Yeye anacheza vizuri.
b) Kobe anaondoka haraka.

**18.Tia sentensi ifuatayo katika wakati uliopita, hali kanushi:(Alama6)**
-Wachezaji wote wanashiriki katika mazoezi.

**SEHEMU YA III: UTUNGAJI. (ALAMA 15)**

**19. a. Sehemu kuu za barua ya kindugu ni ngapi? Ordhesha sehemu hizo.(Alama 5)**

**b.** Andika barua kwa mwanafunzi rafiki yako GAHONGAYIRE Judithe anayesomea katika shule ya jirani inayoitwa GS IKIREZI kwa kupata maagizo ya kielelezo cha barua ya kirafiki. **(alama 10)**

**KAZI NJEMA!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!**